# SHULE YA UPILI YA MARANDA

**Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari**

**KITANGULIZI MWIGO**

**102/3 KISWAHILI (FASIHI) Karatasi ya 3**

**Machi 2022 – Saa: 2½**

---

**Jina : ……………………………………......Nambari yaUsajili: …………..…**

**Mkondo: ………… Sahihi ya mtahiniwa: ……….… Tarehe: …./04/2023.**

---

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

**<u>Maagizo</u>**

a) *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Jibu maswali **manne** pekee.*
c) *Sehemu zote ni **lazima**.*
d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
e) *Karatasi hii ina kurasa **<u>14</u>**. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*
f) *Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

### KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

## SEHEMU A: USHAIRI

**1.** *Soma shairi hili kisha ujibu maswali.*

Mwanadamu mambo yake, kueleweka muhali
Ubavuni umuweke, umtowe kule mbali
Maskanini afike, umtindie fahali
Utamu anufaike, sima, bada au wali
Hatimaye ateuke, kwa viliwa vya samli
*Mwanadamu simuamini, afadhali nyama lumbwi*.

Mwanadamu umjenge, awe mwenye kutajika
Mambo yake uyapange, ukawa wahangaika
Uwashe wake muwenge, uhakikishe wawaka
Nao mkono umuunge, vyake viwe vyaungika
Dhorubani umkinge, asipate kudhurika
Mara atakusahau, wema wako kafukia.

Mwanadamu mpe cheo, kuwa akutumikie
Amani yako umpeo, fanaka uirajue
Kwake iwe kimbilio, wamini akukwamue
Mwisho takuwa kilio, shika sikio ujue
Ndio wake mwelekeo, yuauma avuvie
Mwanadamu mgeuze, pande zote umtizame.

Mwanadamu mfadhili, kwa kila lililo jema
Pasiwe hata dalili, ya kwake kukosa wema
Viteko siwe akali, kumbizo zikaterema
Binadamu takudhili, dhili zako kuzitema
Licha ya zote jamili, mwanadmu si muema
Mwanadamu ni mtu, lakini nusu mnyama

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

a) Onyesha kinaya cha mwanadamu anayezungumziwa. (alama 4)

b) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)

c) Taja na ueleze bahari **nne** za shairi hili. (alama 4)

d) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

e) Onyesha mbinu **nne** alizotumia malenga ili kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (alama 4)

f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 4)

**SEHEMU B: FASIHI SIMULIZI**

**2.** *Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali*

Angole angole mwanangu
Mwanangu nakuchombeza
Nakuchombeza ulale
Ulale ukiamka
Nikupikie ubwabwa
Na mchuzi wa papa
Ukilia waniliza, wanikumbusha
Ukiwa wa baba na mama

Baba na mama watende
Ilimu kunikatizia
Ng'ombe, mbuzi kupokea
Kunioza dumu kongwe
Haliuki na halende
Kazi kupiga matonge

Likingia mvunguni
Lavunjavunja vikombe
Likilala kitandani
Languruma kama gombe

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

a) Bainisha kipera cha utungo huu. Thibitisha. (alama 2)

b) Eleza ujumbe unaofumbwa katika wimbo huu. (alama 5)

c) Tambua mbinu za kifani ambazo zimetumiwa kuwasilisha utungo huu. (alama 3)

d) Bainisha shughuli **mojamoja** ya kijamii na ya kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utungo huu. (alama 2)

e) Unakusudia kukusanya data kuhusu kipera hiki. Eleza manufaa **manne** ya kutumia mahojiano. (alama 4)

f) Kipera hiki kinazidi kufifia katika jamii yako. Fafanua njia **nne** ambazo jamii ya kisasa inaweza kutumia kukuza na kuendeleza kipera hiki. (alama 4)

## SEHEMU C: RIWAYA

**Assumpta K. Matei: Chozi la heri**

**Jibu swali la 3 au 4**

**3.** "Hili ni wingu la kupita na bila shaka wingu la kupita halipaswi kumtia mkulima matumaini. Tutapambana, sheria tunaijua."

a) Bainisha mitindo **sita** inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 6)

b) Bainisha mazaji inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

c) Kwa hoja **kumi na mbili,** onyesha namna jamii ya *Chozi la Heri* ni mfano wa jamii iliokosa ukomavu wa kisiasa. (alama 12)

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

**4.** "Yote haya yamewezekana kutokana na mwongozo mlionipa nyinyi. Zaidi, utulivu nilioupata nilipoambulia familia hii ulinipa msukumo kila mara nilipokabiliwa na ndaro."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Eleza mchango wa mzungumzaji wa maneno haya katika kukuza ploti ya riwaya ya *Chozi la Heri*. (alama 5)

**c)** "Familia ndicho kitovu cha ufanisi wa mtoto maishani." Thibitisha kwa mujibu wa riwaya ya *Chozi la Heri*. (alama 11)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

*D. W. Lutomia na Phibiana Muthama: Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 5 au 6*

**5.**

*Nipe Nafasi – Mzamane Nhlapo*

a) Eleza tafsiri mbalimbali za kichwa cha hadithi hii, '*Nipe Nafasi*' (alama 7)

*Pupa (F. M. Kagwa)*

b) Fafanua umuhimu wa mandhari ya *Chenga-ways* katika kujenga hadithi *Pupa*. (alama 5)

*Toba ya Kalia (Douglas Ogutu)*

c) "Ni kutokana na mchango wako kupitia *twitter* na *facebook* katika maswala mbalimbali ambapo iliamuliwa upewe fursa ya kuzungumza moja kwa moja na watazamaji wetu."

Eleza nafasi ya vijana kwa mujibu wa hadithi *Toba ya Kalia*. (alama 8)

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

**6.**

*Nilitamani (Phibiana Muthama)*

*a)* "Wakati anaongea kwa simu, nikawa najifungua mkanda. Nikafaulu. Nikajaribu kufungua mlango. Duh! Ulikuwa ushatiwa *loki*. Sijui nilipata wapi nguvu za kupitia juu yake! Nikaponyoka pyu! Nikakimbia mguu niponye. Nilikimbia nisijue niendako. Nikakimbia. Sitaki kuangalia nyuma kwa kushtukia yaliyonikuta. Nilikata katikati ya misitu sijui nielekeako ila mbali na Romeo na pepo yake. Nimekaza mwendo huku nahema, pumzi si zangu! "

i. Fafanua aina za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 5)

ii. "Tamaa mbele mauti nyuma." Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi: *Nilitamani*. (alama 7)

*Kifo cha Suluhu – Dominic Maina Oigo*

b) "Aliyaacha machozi yamtoke shibe yake kwani asingeweza kujizuia. <u>Barua ile ilimfichulia siri si haba</u>"

Thibitisha kauli iliyopigwa mstari ukirejelea hadithi *Kifo cha Suluhu*. (alama 8)

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

**a) Onyesha kinaya cha mwanadamu anayezungumziwa. (alama 4)**

- Mwanadamu analinganishwa na lumbwi kumaanisha kuwa anaweza kukugeuka baada ya kumsaidia.
- Binadamu baada ya kuyapanga mambo yake umjenge hadi awe wa kutajika anakuja kukusahau na kufukia wema wako.
- Mwanadamu hata ukampigania hadi akapata cheo kwa nia kuwa akusidie baadaye anakuja kukusababishia kilio.
- Binadamu anakuja kusema dhili zako hata baada ya kumfadhili kwa kila jambo jema hadi akajaa vicheko.

**b) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)**

- Toni ya huzuni - Mwisho takuwa kilio, shika sikio ujue.
- Toni ya majuto – *Mwanadamu simuamini, afadhali nyama lumbwi*
- Toni ya kukashifu - Mwanadamu ni mtu, lakini nusu mnyama

***(1 x 2= 2, kujata =1, maelezo/mfano = 1)***

**c) Taja na ueleze bahari ya shairi hili kwa kurejelea idadi ya mishororo betini. (al. 2)**

- Tasdisa/usita – kila ubeti una mishororo sita.

***d)* Mshairi ana maana gani anaposema "*mwanadamu simuamini, afadhali nyama lumbwi.*" (alama 1)**

- Mwanadamu ni mtu msaliti au kigeugeu. ***(1 x 2= 2)***

**e) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)**

- Inkisari - takuwa – utakuwa. **Dhima - kupata urari wa mizani**
- Kuboronga sarufi
  - Mambo yake uyapange – uyapange mambo yake
  - Uwashe wake muwenge – uwashe mwenge wake
  - Nao mkono umuunge – nao umuunge mkono
  - wema wako kafukia – kafukia wema wako
  - Ndio wake mwelekeo – ndio mwelekeo wake
  - pande zote umtizame – umtizame pande zote.

  **Dhima - kupata urari wa vina.**
- Tabdila - umtowe - umtoe
  - umtizame – umtazame.

  **Dhima - kuleta mahadhi katika shairi / lugha ya kishairi.**
- Mazida
  - umuweke – umweke.
  - Muwenge – mwenge
  - Muema - mwema **Dhima - kupata urari wa mizani**
- Lahaja

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

- umtindie – umchinjie
- viteko – vicheko. **Dhima – kuleta upekee wa lugha ya kishairi.**

- Vikale
  - maskanini . makazi
  - akali – kidogo. **Dhima – kuleta upekee wa lugha ya kishairi.**

*kutaja- ½, mfano- ½, dhima -1 (za kwanza 2 x 2 = al 4)*

**f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 5)**

Mshairi anasema kuwa binadamu licha ya fadhili zote unazoweza kumpa hadi akawa anafurikwa na furaha bado atakusaliti na kusema mabaya kukuhusu. Anamlinganisha binadamu na mnyama.

**"Hili ni wingu la kupita na bila shaka wingu la kupita halipaswi kumtia mkulima matumaini. Tutapambana, sheria tunaijua."**

**Eleza mukatdha wa dondoo hili. (alama 4)**

Haya ni maneno ya mpinzani mwanamume wa Bi. Mwekevu Tendakazi. Ni maneno aliyopita akiyasema njiani ili kuwashajiisha wafuasi wake kupinga Bi. Mwekevu. **4 x 1 = 4**

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

**Bainisha tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)**

Methali - wingu la kupita halipaswi kumtia mkulima matumaini.
Kinaya - kauli ya mpinzani wa Bi. Mwekevu kuwa "sheria tunaijua" ni kanaya kwani anasema anaijua sheria na wakati huohuo kushikilia msimamo kuwa mwanamke kuwa kiongozi wa nchi ni maonevu makubwa kwa mwanamume.
Jazanda- wingu la kupita – ni urahisi wa kumwondoa Bi. Mwekevu mamlakani.

**Za kwanza 2 x 2 = 4**

**Taja na ueleze maudhui yoyote mawili yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)**

Siasa duni - mpinzani wa Bi. Mwekevu anakataa kukubali ushinde.
Ubabeduni - mpinzani wa Bi. Mwekevu anashikilia msimamo kuwa mwanamke kuwa kiongozi wa nchi ni maonevu makubwa kwa mwanamume.
Kutowajibika- mpinzani wa Bi. Mwekevu anakataa kukubali ushinde.
Uongozi mbaya - mpinzani wa Bi. Mwekevu anakataa kukubali ushinde.

**Onyesha namna jamii ya *Chozi la Heri* ni kielelezo cha jamii iliokosa ukomavu wa kisiasa. (alama 10)**

1. Ubaguzi katika ngazi za uongozi - Wafuasi wa mpinzani mwanamume wa Mwekevu wanashikilia msimamo kuwa mwanamke ni chombo duni na hawezi kushinda katika uchaguzi.
2. Kutokubali ushinde - mpinzani wa Bi. Mwekevu anakataa kukubali ushinde. Anashindwa kuelewa kuwa katika ushindani kuna kushindwa na kushinda.

3. Kupiga kura bila kuzingatia sera za mgombea uchaguzi bali vizawadi vyake. Bi kizee anataka kuchagua Papa bali si Kiboko kwa kuwa alitoa hela na kibaba cha unga.
4. Ufisadi katika uchaguzi - Vijana wanasukumizwa na wanasiasa katika vitendo vya ufisadi kama vile wizi wa kura katika vituo vya kupigia kura. Vijana hao huishia kuwahadaa vikongwe ambao hawaelewi vizuri alama za wagombea wanaotaka kuwapigia kura.
5. Uchochezi/uhasama wa kisiasa. Mpinzani wa Mwekevu anapokosa ukomavu wa kisiasa na kukubali kushindwa anapelekea kuzuka kwa vita vya baada ya uchaguzi.
6. Ghasia za baada ya uchaguzi. Vijana wanatumiwa na wanasiasa katika kushinikiza ushindi wao. Wanashawishiwa kushiriki katika maandamano ambapo wengi wao wanakufa kwa kupigwa risasi.
7. Wanasiasa kutoa ahadi hewa. Katika nyakati za uchaguzi wagombea wanawatumia vijana kwa kuwaahidi pesa na ajira. Hizi zinakuwa kichocheo cha vijana kutafuta kila njia kuhakikisha viongozi wao wanaingia madarakani. Wakishachaguliwa hawatimizi ahadi hizo.
8. Ukosefu wa elimu kwa wapiga kura / namna ya kupiga kura. Vijana kuwahadaa vikongwe ambao hawaelewi vizuri alama za wagombea wanaotaka kuwapigia kura na kuishia kuwapigia kura wagombeaji wasiowataka.
9. Kufanya maandamano kwa kuharibu mali ya watu. Vijana wanakosa kujitambua na kuingia katika mitego ya wagombea uchaguzi ili kufanikisha malengo ya wagomgea hao – mgonjwa Ridhaa aliyeitwa kumfanyia upasuaji.

**Zozote 5 x 2 = 10**

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content